MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu



Mchango wa Kinandi katika Kuihamasisha Jamii kuhusu Ustawi wa Kilimo Kupitia Vipindi vya Runinga ya KASS

Melly Kipchirchir*, Sangai Mohochi, Eric Wamalwa

Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kibabii, Bungoma, Kenya.

IKISIRI

Moja kati ya ajenda kuu za serikali ya sasa ya Kenya ni ustawi wa kilimo ambao huleta utoshelevu wa chakula na hivyo kuchangia katika kupunguza gharama ya maisha. Wakulima wengi nchini humo hupatikana katika maeneo ya mashambani ambako mawasiliano mengi huwa katika lugha za kiasili. Wakati uo huo vyombo vya habari ni miongoni mwa asasi ambazo zimechangia pakubwa katika kukuza matumizi ya lugha za kiasili na kuwahamasisha wananchi kuhusu kilimo. Lugha ya Kinandi ambayo hutumiwa katika runinga ya Kass, ni mojawapo ya lugha za kiasili nchini Kenya. Utafiti huu ulilenga kuchunguza mchango wa lugha ya Kinandi katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass. Utafiti ulifanyika katika kaunti ya Nandi. Uliongozwa na Nadharia ya Ethnografia ya Mawasiliano ya Hymes (1972). Watazamaji waliteuliwa kinasibu ili kuhusishwa katika utafiti. Watazamaji 264 walihusishwa katika ukusanyaji wa data. Isitoshe watangazaji 9 vilevile walihusishwa. Mbinu za hojaji, uchunzaji na mahojiano zilitumika katika kukusanya data. Vifaa vilivyotumika kukusanya data ni: mwongozo wa utazamaji, hojaji na mwongozo wa maswali ya mahojiano. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kimaelezo kisha ikawasilishwa kwa kutumia asilimia na majedwali. Utafiti huu unatarajiwa kuwa wa manufaa kwa wanajamii kwa kuwa ulitoa mwanga kuhusu jinsi wanajamii huhamasishwa kuhusu ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya kilimo katika runinga ya KASS.

KUHUSU MAKALA

Maneno Muhimu:
Uhakiki-maeneo,
Ukweli,
Bunilizi.

Historia ya Makala:
Tarehe ya Kutumwa: 4 Aprili 2025
Tarehe ya Kurekebishwa: 2 Juni 2025
Tarehe ya Kukubalika: 14 Juni 2025
Mtandaoni: 29 Agosti 2025

1. Utangulizi

Kazi Vyombo vya habari hutekeleza wajibu muhimu katika uhamasishaji wa umma kuhusu mambo muhimu katika jamii. Miongoni mwa mambo hayo ni mipango ya serikali ya kuinua maisha ya wananchi. Mojawapo ya mhimili mkuu wa serikali ya Kenya ni uimarishaji wa kilimo ili kuhakikisha kuwepo kwa utoshelevu wa chakula. Kilimo kilianza tangu jadi za mababu wetu. Hata hivyo, wakati huo kilimo kilikuwa cha jamii za jadi na uzalishaji mali na mifugo kwa jamii tu na wala si njia nyingine (Mutenyo, 2022). Jamii ambayo ilikuwa na mifugo wengi na chakula kingi ndiyo ilijulikana kuwa jamii ya kifahari. Mutenyo (2022) anasema kuwa, kwa wale waliozalisha chakula kingi jamii ingewategemea sana. Hata hivyo baada ya ukoloni wananchi wa Afrika Mashariki, Kenya ikiwemo, walijihusisha na kilimo sio kwa ajili ya familia tu bali katika maendeleo ya uzalishaji mali na biashara. Hali hii imepelekea kuwepo kwa mbinu tofauti tofauti za kilimo kwa ajili ya uzalishaji mali na kujikimu kimaisha (Mutenyo, 2022). Ili kuwasilisha maudhui ya kilimo sharti kuwepo kwa mawasiliano. Mawasiliano hayo yatawezeshwa kwa kutumia lugha.

Serikali ya Kenya imejitahidi katika kuwapa maarifa wakulima kupitia vyombo vya habari. Hata hivyo, maarifa mengi yanatolewa katika lugha ya Kiswahili na Kingereza. Kwa mfano kipindi cha Shamba shape up katika runinga ya Citizen hutolewa kwa lugha ya Kiswahili huku My perfect farm katika runinga ya KTN kikitolewa kwa lugha kwa Kingereza. Lugha za kiasili zinapaswa kupewa nafasi pia. Swali tunalojiuliza ni; je iwapo lugha za kiasili zitatumika kuwapa wasikilizaji na watazamaji maarifa kupitia vyombo vya habari vinavyotumia lugha za kiasili, matokeo yatakuwa yepi?

Sekta ya kilimo ni uti wa mgongo wa ukuaji wa uchumi katika nchi ya Kenya (Samoei, 2015). Ajenda kuu ya serikali ya sasa ya Kenya ni kuinua viwango vya kilimo ili kuhakikisha kwamba kuna utoshelevu wa chakula na hivyo kupunguza gharama ya maisha. Hali hii inadhihirika katika mgao wa bajeti uliopewa Wizara ya Kilimo. Kwa mujibu wa hazina ya kitaifa, sekta ya kilimo ilipata mgao wa shilingi bilioni 84.9 katika bajeti ya mwaka 2023-2024. Serikali imeahidi kwamba bajeti ya kilimo ya mwaka huu itaongezeka zaidi kuliko ya mwaka jana.

*Mwandishi Mkuu. Simu: +254720788749. Barua Pepe: mellyjoachim@gmail.com

Mhariri: Benard Odoyo Okal; Chuo Kikuu cha Maseno, Kenya.

Nukuu: Melly K., Sangai M., Eric W. (2025). Mchango wa Kinandi katika Kuihamasisha Jamii kuhusu Ustawi wa Kilimo Kupitia Vipindi vya Runinga ya Kass. Jarida la Kiswahili Sanifu, 2(2), 1 – 10.

© 2025 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

Hali hii inadhihirisha umuhimu wa kilimo nchini. Serikali vilevile imehakikisha kwamba kuna ruzuku ya mbolea ili kuwaongezea mapato wakulima na kuhakikisha kuwa bei za bidhaa muhimu zinapunguzwa. Katika mgao wa bajeti, shilingi bilioni 8.8 ulienda katika ushirikishwaji wa wakulima wa mashambani. Mgao huu wa ushirikishwaji wa wakulima wa mashambani unadhihirisha kuwa serikali inafahamu kuwa kilimo hutekelezwa zaidi katika maeneo ya mashambani. Wazungumzaji wengi wa lugha za kiasili hupatikana katika maeneo ya mashambani. Swali ni: je, ushirikishwaji wa wakulima wa mashambani huweza kufanikishwa kwa kutumia lugha za kiasili kupitia vyombo vya habari vinavyotumia lugha hizi?

2. Lugha za Kiasili katika Vyombo vya habari

Lugha na kilimo huwa na uhusiano wa moja kwa moja. Hii ni kwa sababu mawasiliano huhitajika ili kufanikisha maendeleo katika kilimo. Kupitia kwa matumizi ya lugha katika vyombo vya habari, wakulima wanaweza kupata ujumbe wa maendeleo kuhusiana na kilimo. Mawasiliano haya yanaweza kufanywa kwa kutumia lugha za kiasili ili kuhakikisha kuwa wakulima wengi wanapokea mawasiliano hayo.

Lugha za kiasili zinatumika katika vyombo vya habari kuwasilisha masuala ya kijamii. Misiko (2018) alifanya utafiti katika vituo vya redio vya Sulwe FM na West FM vinavyopeperusha matangazo katika kaunti ya Bungoma kwa kutumia lugha ya Kibukusu. Katika utafiti wake, alihakiki yaliyomo katika vipindi kuhusu masuala ya jamii, uchumi, siasa na afya vinavyowasilishwa katika redio za FM. Isitoshe alipambanua changamoto za matumizi ya Kibukusu kama rasilmali kwa wakaazi wa kaunti ya Bungoma. Utafiti huu uliweza kugundua kwamba kuna masuala mengi yanayoangaziwa katika redio za FM kwa kutumia lugha za kiasili. Ilibainika kwamba masuala hayo yaliangaziwa kupitia vipindi vya jamii, uchumi, siasa na afya. Kutokana na kuwepo kwa masuala hayo, wasikilizaji wa vituo hivyo walivifurahia huku wakiwa na imani na vituo hivi vya redio (Misiko, 2018). Hali hii inadhihirisha kuwa lugha za kiasili zinapotumika katika vyombo vya habari huweza kuwahamasisha watazamaji na wasikilizaji kwa kuwa wana imani navyo. Imani hii huweza kuwachochea katika shughuli za maendeleo.

Akikubaliana na Misiko (2018), Kinoti (2021) anasema kuwa, umaarufu wa vyombo vya habari umedhihirika hasa katika maeneo ya mashambani kwani vipindi vyake hutoa burudani na mafunzo muhimu kwa lugha zinazoeleweka na wengi. Idhaa nyingi huinufaisha hadhira yake katika masuala ya elimu, siasa, utamaduni, mazingira, dini na afya. Kwa mfano kipindi, cha Murimi Caruruku (Mkulima Shupavu) kwenye runinga ya Weru huwashirikisha wakulima na wafugaji katika majadiliano kuhusiana na ufanisi na changamoto wanazopitia katika shughuli zao (Kinoti, 2021).

Vyombo vya habari huwa na usikilizaji mpana unaoweza kutumiwa kama njia ya kuwashirikisha watu katika mawasiliano yanayohusisha lugha za kiasili. Kandagor & Toboso (2021) wanadokeza kuwa, vyombo vya habari huwa na vipindi vya mazungumzo ya kidayolojia yanayoshirikisha mashabiki kupitia kwa simu. Kupitia vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass, watazamaji na wasikilizaji wanaweza kushirikishwa pia ili kusisitiza kilimo kama njia muhimu ya kujiendeleza.

Aidha, Samoei (2015), akiangazia mchango wa redio ya Kass katika kuinua usalama wa chakula miongoni mwa jamii ya Tugen katika eneo la Perkerra, anasema kuwa, redio zinazotumia lugha za kiasili huwa muhimu sana katika kuhamasisha jamii kuhusu utoshelevu wa chakula katika maeneo ya mashambani. Kupitia vyombo vya habari vinavyotumia lugha za kiasili waliosoma na wasiosoma wanapata elimu kuhusu mbinu za kujistawisha katika kilimo ili kuinua usalama wa chakula mingoni mwao. Kwa mujibu wa Samoei (2015), ujumbe unaopatikana katika redio ya Kass huwasaidia wananchi wa eneo la Perkerra kuelewa umuhimu wa lishe bora. Redio ya Kass iliwapa wanajamii wa Perkerra fursa ya kujifunza kupanda mimea ambayo hustahimili kiangazi kinachoshuhudiwa katika maeneo hayo. Kwa hivyo redio ya kass ni rasilmali kwa wanajamii wanaoishi katika eneo la Perkerra kwa kuwa huwasaidia kupata elimu kuhusu kilimo bora.

Ni dhahiri kuwa taarifa za kila siku zilizotolewa na Wizara ya Afya nchini Kenya kuhusiana na idadi ya watu waliopimwa, walioambukizwa, waliopata nafuu na waliofariki pamoja na mikakati ya serikali ya kupambana na virusi vya Korona zilikuwa katika lugha ya Kingereza (Kinoti, 2021). Hata hivyo palikuwepo na nafuu kwa wananchi wengi waliokosa kuelewa Kingereza kwani maelezo mafupi yalianza kutolewa kwa Kiswahili mwishoni mwa hotuba rasmi kutokana na malalamiko ya wanahabari wanaotangaza kwa Kiswahili. Vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili, vilihakikisha kuwa habari hizi zinawafikia wanajamii. Hii ina maana kuwa vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili viliwafaa sana wanajamii katika kuwahamasisha kuhusu janga la Korona. Kando na kuhamasisha wananchi kuhusu janga la Korona, kuna mengi ambayo vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili huweza kuchangia katika kuwahamasisha wanajamii. Mojawapo ni sekta ya kilimo ambayo huchangia katika kuleta utoshelevu wa chakula na kupunguza gharama ya maisha. Kilimo kinapaswa kuhimizwa hasa kwa kutumia vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili.

Hata baada ya kuchangia katika maendeleo ya jamii kwa kutumia lugha za kiasili, vyombo vya habari vinakumbwa na changamoto na madai kuwa vinaeneza ukabila na chuki miongoni mwa wakenya. Okoth (2015), anasema kuwa, katika uchunguzi uliofanywa na shirika la utangazaji la Uingereza (BBC) mwaka 2005, kulikuwa na hofu kuwa vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili vilitumika kueneza chuki za kikabila mwaka 2006 kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007. Idhaa za redio zilizotajwa katika uchunguzi huu ni Kass, Lake Victoria na Inooro. Idhaa hizi za redio ziliwahamasisha wanajamii husika kuwaunga mkono wagombea wanaotoka katika jamii zao. Tume ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KHRC) (2008) inadokeza kuwa, matamshi ya kuchochea ghasia na nyimbo katika vyombo

vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili yalichangia katika vita vya baada ya uchaguzi 2007. Idhaa zilizotajwa katika ripoti ya KHRC (2008) ni Kameme, Kass, Inooro na Lake Victoria. Hata hivyo, kwa mujibu wa Okoth (2015), idhaa hizi zimebadilika na kwa sasa zinatumika kuhimiza uchaguzi wa amani na kuchochea umoja baina ya Wakenya wote. Vilevile zinatumika katika kuwachochea wanajamii kujiendeleza katika nyanja mbalimbali za ukuaji wa binadamu.

Ugunduzi wa Misiko (2018) katika utafiti wake, ni kuwa, lugha za kiasili hazitumiki katika uandishi wa magazeti ya kitaaluma. Serikali ya Kenya haiungi mkono lugha za kiasili kama njia ya kupasha habari kwa umma kwa hofu ya kusababisha tofauti za kikabila. Kutokana na msimamo huo, serikali nchini Kenya imekuwa ikiviziza ukuaji wa matumizi ya lugha za kiasili. Hata hivyo, uhuru wa vyombo vya habari umeweza kusaidia katika ongezeko la vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili. Misiko (2018), anaendelea kuthibitisha kuwa, ingawa vituo vya redio za kibinafsi vya FM vimechangia pakubwa kueneza matumizi ya lugha za kiasili, sera ya lugha katika vyombo vya habari kama vile KBC inahimiza zaidi matumizi ya Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo, kwa mujibu wa Misiko (2018) mnamo mwaka 2015, kumekuwa na ongezeko la vituo vya redio vinavyotumia lugha za kiasili huku Royal Media Services ikiongoza kwa idadi ya vituo vinavyotumia lugha za kiasili kwa kuwa na vituo 12 vinavyotangaza kwa lugha za kiasili. Kando na ongezeko la vituo vya redio za FM zinazotumia lugha za kiasili, vituo vya runinga vinavyotangaza kwa lugha za kiasili vilevile vimeongezeka.

Maendeleo katika uandishi wa habari na uchapishaji yatawezekana tu iwapo lugha za kiasili na tamaduni zake zitapewa nafasi kukua na kuchangia maendeleo (Muthwii, 2002). Lugha za kiasili zinapotumika, hadhira ya uandishi habari na uchapishaji itaongezeka kwa vile jamii isiyo na umilisi wa lugha za kigeni itaweza vilevile kuhusishwa. Akithibitisha maelezo ya Muthwii (2002), Misiko (2018) anasema kuwa, kuanzishwa kwa vituo vya redio vya FM vinavyotumia lugha za kiasili kunaweza pia kuchangia maendeleo hayo kwa vile, hadhira isiyo na umilisi katika lugha zingine kama vile Kiswahili na Kiingereza itahusishwa katika maamuzi yanayohusu jamii hizo. Kwa mujibu wa Misiko (2018), matumizi ya lugha hizi za kiasili yatawezesha wakaazi hasa wa mashambani kupata maarifa kwa lugha wanazoelewa.

2.1. Kinandi katika Runinga ya KASS

Kinandi ni lugha ya Kinilo-sahara nchini Kenya inayozungumzwa na Wanandi, kabila moja la Wakalenjin. Mwaka 2019 idadi ya wasemaji wa Kinandi ilihesabiwa kuwa watu 885,711. Kufuatana na uanishaji wa lugha, lugha ya Kinandi iko katika kundi la Kinilotiki. Wazungumzaji wengi wa lugha ya Kinandi wanapatikana katika kaunti za Nandi na Uasin Gishu.

Runinga ya Kass, ilianzishwa mwaka wa 2013. Makao yake makuu yapo mji wa Nairobi lakini wasikilizaji wengi wanapatikana katika eneo la Bonde la Ufa. Runinga hii hupeperusha vipindi vyake kwa lugha ya Kinandi. Kutokana na sababu kwamba runinga ya Kass hupeperusha vipindi vyake kwa kutumia lugha ya kiasili basi huwavutia wasikilizaji wengi wanaoishi mashambani. Vipindi vya kilimo vinavyopeperushwa katika runinga ya Kass kwa kutumia lugha ya Kinandi ni kama vile; Tugeet ab Kabatik (Sauti ya Mkulima), Mungaret ab bandaptai (Kilimo Biashara na Maendeleo) Longeet ab Kabotik (Mkuki wa Mkulima), Boishonik ab Keljin (Kazi zenye Faida), Temisiet ab chai (Ukulima wa Chai), Baet ab Kiyakiik (Ufugaji wa Mifugo) na Minet ab pandek (Upanzi wa Mahindi).

2.2. Nadharia ya Utafiti

Nadharia ambayo ilitumika katika utafiti huu ni nadharia ya Ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972). Kwa mujibu wa Dell Hymes, ili mtu afaulu katika kuwasiliana na mwingine, anahitaji kuimarika zaidi kimawasiliano bali si kiisimu pekee. Dell Hymes anaeleza kuwa ethnografia ya mawasiliano ni uamilifu wa maarifa na uwezo wa kudhibiti matumizi ya lugha. Alipendekeza nadharia hii ili kuwasaidia watafiti wanaochunguza matumizi ya lugha katika miktadha fulani. Tangu kuasisiwa, nadharia ya ethnografia ya mawasiliano imetumika kuchunguza lugha na mawasiliano katika miktadha halisi ya utangamano wa wanajamii, mwingiliano wa viambajengo mbalimbali vya mawasiliano, miktadha ya kijamii ambamo lugha hutumika na athari ya matumizi ya aina mbalimbali ya lugha katika mawasiliano.

Kwa mujibu wa nadharia hii ethnografia ya mawasiliano, mawasiliano ni uamilifu wa maarifa na uwezo wa kudhibiti matumizi ya lugha. Mtumiaji wa lugha hapaswi tu kutumia lugha kwa msingi wa umilisi wa kiisimu bali pia atumie lugha ipasavyo kwa msingi wa umilisi kimawasiliano. Madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana kwani lugha ni mfumo wa kueleza maana. Utafiti ulizingatia nadharia hii kwa kuwa chochote kinachofanyika katika jamii lazima kuwepo na mawasiliano. Mawasiliano huhusisha matumizi ya lugha. Kwa hivyo, ili kuwepo kwa ustawi wa kilimo, lazima kuwepo kwa njia madhubuti ya mawasiliano.

Nadharia ya ethnografia ya mawasiliano ina mihimili sita. Mihimili hii ni ifuatayo;

i. Madhumuni makuu ya lugha ni kuwasiliana kwani lugha ni mfumo wa kueleza maana.
ii. Matamshi yanayoeleweka na watu wengi katika mazungumzo ndiyo lengo kuu la matumizi ya lugha.
iii. Jukumu muhimu la matumizi ya lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha maalum.
iv. Lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano.
v. Vipashio muhimu vya lugha sio vile vya kisarufi na kimuundo tu lakini pia vile vya kimawasiliano.
vi. Kanuni za kisarufi na mbinu nyinginezo zinatumiwa inapoonekana kuwa ni lazima.

Utafiti huu ulizingatia mhimili wa pili, tatu na nne. Mihimili hii ilisaidia utafiti kwa njia zifuatazo;

Matamshi yanayoeleweka na watu wengi katika mazungumzo ndiyo lengo kuu la matumizi ya lugha.

Lugha za kiasili hueleweka baina ya watu wengi. Mawasiliano huwa bora ikiwa lugha inayoeleweka baina ya watu wengi itatumiwa. Lugha za kiasili zinazoeleweka baina ya watu wengi zinapotumiwa katika vyombo vya habari, watu wengi hupata ujumbe kwa njia rahisi. Mhimili huu ulisaidia kuchunguza jinsi lugha ya Kinandi hutumika kuhamasisha wanajamii kuhusu ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass.

Jukumu muhimu la matumizi ya lugha ni mawasiliano yanayofaa katika muktadha maalum. Mhimili huu ulisaidia utafiti kupima jinsi lugha ya Kinandi inayotumika katika runinga ya Kass hutumika kuhamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya kilimo.

Lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano. Lugha ya Kinandi inayotumika katika runinga ya Kass hueleweka zaidi kwa wanajamii wa kaunti ya Nandi. Utafiti ulitumia mhimili huu kubaini jinsi lugha ya Kinandi hujitokeza kama nyenzo muhimu katika kuhamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo.

3. Mbinu za Utafiti

Mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni kama zifuatazo: Hojaji, utazamaji na usikilizaji wa vipindi na mahojiano. Data iliyokusanywa ilihusu mchango wa matumizi ya lugha ya Kinandi katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo. Hojaji ilitumika katika utafiti huu kwani ilimpa mtafitiwa uhuru wa kutoa maoni na mapendekezo yake. Hojaji hizi ziliwasilishwa moja kwa moja kwa watafitiwa ili kuhakikisha kuwa hojaji zinawafikia walengwa. Lengo la kuwasilisha moja kwa moja ni kupunguza muda wa kukusanya data inayohitajika (Ary na Wenzake, 1972).

Hojaji ziliandaliwa kwa lugha ya Kiswahili na Kinandi kwa wasailiwa ambao hawamudu lugha ya Kiswahili. Kabla ya kuwapa hojaji watafitiwa, mtafiti aliwaeleza lengo la utafiti na kuwahakikishia kwamba habari ambazo wangetoa zingehifadhiwa kuwa siri wakati na baada ya utafiti. Ingawa lengo la utafiti na hakikisho la uwekaji wa siri zinapaswa kuwepo katika utangulizi wa hojaji zote, mtafiti anapaswa kuchukua jukumu la kuwafahamisha hayo kwa mazungumzo. Waliohusishwa katika ujazaji wa hojaji ni watazamaji na wasikilizaji na watangazaji wa runinga ya Kass. Maswali katika hojaji yalihusu mchango wa matumizi ya lugha ya Kinandi katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo.

Mwongozo wa utazamaji ulitumika kuchunguza yaliyomo kwenye vipindi vya kilimo na kukusanya taarifa. Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kufahamu yaliyomo katika vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass na baadaye kuchanganua. Kwa kutazama, mtafiti aliweza kufahamu nyakati ambazo vipindi hivyo vya kilimo huwasilishwa. Utazamaji huu vilevile ulimwezesha mtafiti kuwanasa wanaopiga simu na kuwahusisha katika kukusanya data.

Mahojiano yalitumika katika kupata data kutoka kwa watangazaji 9 wa runinga ya Kass. Watangazaji hawa 9 walikuwa asilimia 30 ya watangazaji wote wa runinga ya Kass. Mahojiano vilevile yalitumika kupata data kutoka kwa watazamaji wa runinga ya Kass nyanjani. Anavyopendekeza Misiko (2018), mbinu ya mahojiano ilifaa katika utafiti huu kwa kuwa maswali ambayo hayakuwa yamejibiwa kwa utoshelevu katika hojaji yalifafanuliwa barabara katika mahojiano.

4. Matokeo na Mjadala

4.1. Sifa za Wasailiwa

Sehemu ya kwanza ya hojaji ilihusu sifa za watafitiwa. Sifa hizi zilikuwa za watangazaji na watazamaji. Kwa hivyo sehemu hii inawasilisha sifa za watangazaji.

4.2. Sifa za Watangazaji

Sehemu ya kwanza ya hojaji ya watangazaji ililenga kupata taarifa za msingi kuwahusu watangazaji wa vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass. Miongoni mwa taarifa walizopaswa kutaja ni: tajriba ya miaka katika taaluma ya utangazaji wa masuala ya kilimo, vikundi vya watazamaji wanavyowalenga katika vipindi vyao vya kilimo na kipindi cha kilimo ambacho kila mtangazaji hushiriki.

4.2.1. Tajriba ya Watangazaji

Mtafiti alilenga kubaini tajriba ya watangazaji wa runinga ya Kass katika utangazaji wa vipindi vya kilimo. Lengo la kufanya hivi lilikuwa ni kujua uzoefu wa matumizi ya Kinandi miongoni mwa watangazaji katika kuwasilisha vipindi vya kilimo kama inavyodahili nadharia ya ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972) kwamba, umilisi wa kuwasiliana kwa kutumia lugha hutegemea uzoefu wa mzungumzaji katika kuitumia lugha. Kwa hivyo watangazaji tisa walilijibu swali la kwanza kwenye hojaji ya mtangazaji. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 1.

Jed. 1: Tajriba ya Watangazaji

Tajriba	Watangazaji	Asilimia
0-5	3	33.33
6-10	6	66.67
11-15	0	0
Zaidi ya 15	0	0
Jumla	**9**	**100**

Matokeo ya utafiti katika Jed. 1 kuhusu tajriba ya watangazaji wa kilimo katika runinga ya Kass yalibainisha kuwa asilimia 33.33 (N=3) ya watangazaji wana tajriba ya miaka kati ya 0-5 katika utangazaji wa vipindi vya kilimo huku asilimia 66.67 (N=6) wakiwa na tajriba ya miaka kati ya 6-10. Matokeo haya yanathibitisha kuwa watangazaji wa kilimo katika runinga ya Kass wana tajriba ya kutosha. Kwa hivyo ilikisiwa kuwa wana umilisi wa kutosha wa kuwasiliana kwa lugha ya Kinandi na kurahisisha ukusanyaji wa data kama asemavyo Raitania (2014). Kwa mujibu wa Raitania (2014) mazungumzo ya Bi Msafwari katika runinga ya citizen hufanikiwa kutokana na tajriba ya Bi Msafwari katika masuala ya ushauri na nasaha na vilevile umilisi wake wa lugha ya Kiswahili.

4.2.2. Vikundi vya Watazamaji Vinavyolengwa

Mtafiti vilevile alilenga kubaini vikundi vya watazamaji vinavyolengwa na vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass. Kwa kufanya hivi, mtafiti alihakikisha kuwa anawalenga watazamaji ambao vipindi vya kilimo

vinawalenga. Hali hii ilirahisisha ukusanyaji wa data kwa kufuata malengo ya utafiti. Kwa hivyo, watangazaji walilijibu swali la pili kwenye hojaji ya mtangazaji. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 2 lifuatalo:

Jed. 2: Vikundi vya Watazamaji Vinavyolengwa

Kikundi	Nambari	Asilimia
Wakulima	5	55.56
Wafugaji	3	33.33
Wafanyi biashara	1	11.11
Jumla	**9**	**100**

Matokeo katika Jed. 2 kuhusu vikundi vya watazamaji vinavyolengwa katika vipindi vya kilimo vya runinga ya Kass yalibaini kuwa asilimia 55.56 (N=5) ya watangazaji walikiri kuwalenga wakulima huku asilimia 33.33 (N=3) wakiwalenga wafugaji katika vipindi vyao. Isitoshe, asilimia 11.11 (N=1) ya vipindi vya kilimo viliwalenga wafanyibiashara. Kutokana na matokeo haya ni bayana kuwa vipindi vya kilimo viliwalenga aghalabu wakulima na wafugaji. Matokeo haya yanaonyesha kuwa ukulima na ufugaji hutiliwa mkazo zaidi katika kuwasilisha vipindi vya kilimo. Hii ina maana kuwa vipindi vya ukulima na ufugaji vinachangia pakubwa katika ustawi wa jamii haswa watazamaji wa vipindi vya kilimo katika kaunti ndogo ya Emgwen. Isitoshe, matokeo haya yanaoana na matokeo ya Okoth (2015) aliyebaini kuwa idhaa ya redio ya Ramogi huwasilisha vipindi vya kilimo na ufugaji kwa viwango vya juu ili kuhakikisha kuwa watazamaji wanafaidika zaidi.

4.2.3. Kipindi Mahususi cha Kilimo ambacho kila Mtangazaji Huwasilisha

Baada ya kutumia mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo kubaini vipindi vya kilimo vinavyowasilishwa katika runinga ya Kass, mtafiti alitaka kujua watangazaji wa vipindi mahususi. Lengo la kufanya hivi ni kuthibitisha yaliyokuwa yamebainika kupitia mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo na mwongozo wa mahojiano. Kwa hivyo watangazaji tisa walilijibu swali la tatu kwenye hojaji ya mtangazaji. Matokeo yanawasilishwa kupitia Jed. 3 lifuatalo:

Jed. 3: Kipindi Mahususi cha Kilimo ambacho kila Mtangazaji Huwasilisha

Kipindi	Mtangazaji	Asilimia
Tugeet ab Kabotik (Sauti ya Mkulima)	2	22.22
Mungaret ak bandaptai (Kilimo biashara na maendeleo)	1	11.11
Longet ab Kabotik (Mkuki wa mkulima)	3	33.33
Baet ab Kiyakiik (Ufugaji bora wa mifugo)	1	11.11
Boishonik ab Keljin (Kazi zenye faida)	2	22.22
Minet ab bandek (Upandaji wa mahindi)	1	11.11
Temisiet ab Chaik (Upandaji wa miche ya chai)	1	11.11
Mosoknatet eng Kabatisiet (Teknolojia katika kilimo)	2	22.22
Jumla	**9**	**100**

Matokeo ya utafiti katika Jed. 4 yalibainisha kuwa asilimia 22.22 (N=2) ya watangazaji walihusika katika utangazaji wa kipindi cha Tugeet ab Kabotik (Sauti ya Mkulima) huku asilimia 11.11 (N=1) wakihusika katika utangazaji wa kipindi cha Mungaret ak Bandaptai (Kilimo biashara na maendelo). Aidha, asilimia 33.33 (N=3) ya watangazaji walikubali kuwa, wao huhusika katika utangazaji wa kipindi cha Longet ab Kabotik (Mkuki wa Mkulima).

Baet ab Kiyakiik (Ufugaji bora wa mifugo) kiliwasilishwa na mtangazaji mmoja pekee huku kipindi cha Boishonik ab Keljin (Kazi zenye faida) ikiwasilishwa na asilimia 22.22 (N=2) ya watangazaji. Wakati uo huo asilimia 11.11 (N=1) ya watangazaji walihusika na uwasilishaji wa kipindi cha Temisiet ab Chaik (Upandaji wa Miche ya Chai). Hatimaye asilimia 22.22 (N=2) ya watafitiwa walihoji kuwa wao huhusika katika kipindi cha Mosoknatet eng Kabatisiet (Teknolojia katika Kilimo).

Kutokana na matokeo haya, ilibainika kuwa kuna watangazaji waliohusika katika uwasilishaji wa vipindi zaidi kimoja huku wengine wakiwasilisha kipindi kimoja pekee. Ilibainika kuwa watangazaji waliowasilisha vipindi zaidi ya kimoja walikuwa na tajriba zaidi katika sekta hiyo ya utangazaji. Hali hii iliwapa watazamaji imani miongoni mwa watangazaji hawa.

4.3. Sifa za Watazamaji

Kando na sifa za watangazaji, utafiti vile vile ulilenga kubaini sifa za watazamaji. Katika kuchunguza sifa za watazamaji, utafiti ulizingatia lugha wanazozimudu watazamaji, kilimo wanachojihusisha nacho watafitiwa na vipindi vya kilimo wanavyovipendelea watafitiwa.

4.3.1. Lugha Wanazozimudu Watazamaji

Kabla ya kukusanya data kuhusu lugha ya Kinandi, mtafiti alitaka kufahamu iwapo watafitiwa wanafahamu lugha ya Kinandi ama Kiswahili au zote mbili. Lengo la kufanya hivi ni kurahisisha mawasiliano wakati wa ukusanyaji wa data kama inavyoelekeza nadharia ya ethnografia ya mawasiliano. Sehemu ya kwanza ya hojaji ilikuwa na swali funge lililomhitaji mtazamaji kuweka alama kwenye kisanduku kilichoonyesha lugha anayoimudu. Visanduku vilikuwa na Lugha ya Kinandi, Kiswahili na lugha zote mbili. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 4 lifuatalo.

Jed. 4: Lugha Wanazozimudu Watafitiwa

Lugha	Idadi	Asilimia
Kinandi pekee	7	2.65
Kiswahili pekee	2	0.75
Zote mbili	255	96.59
Jumla	**264**	**100**

Taarifa Jed. 4, ilithibitisha kuwa, asilimia 2.65 (N=7) ya watafitiwa walifahamu lugha ya Kinandi pekee. Hali hii ilitokana na uwepo wanajamii ambao hawakufanikiwa kupata elimu. Nayo asilimia 0.75 (N=2) ya watafitiwa walithibitisha kuwa wanafahamu lugha ya Kiswahili peke huku asilimia 96.59 (N=255) ikikubali kuwa wanazimudu lugha zote mbili. Lugha hizi ni Kiswahili na Kinandi. Ni

dhahiri kwamba asilimia kubwa ya wakaazi wa kaunti ndogo ya Emgwen wanazimudu lugha zote mbili.

Kwa hivyo lugha hizi mbili zinatumika kufanikisha mawasiliano baina ya wakaazi hawa. Lugha hizi zinatumika katika hali halisi ya kiutendaji katika muktadha wa kijamii. Kutumika kwa lugha hizi katika mawasiliano kunaafikiana na maoni ya Hymes (1972) katika nadharia ya ethnografia ya mawasiliano kwamba ili mzungumzaji awe na umilisi kamili wa mawasiliano lazima awe na uwezo wa kiutendaji katika lugha husika yaani awe na uwezo wa kuitumia lugha ile katika miktadha ya kijamii.

4.4. Kilimo Wanachojihusisha Nacho Watafitiwa

Tabia nchi ya Kaunti ndogo ya Emgwen iliyoko kaunti ya Nandi huwapa fursa wakulima kujihusisha katika ukulima wa mimea mbalimbali na kufuga mifugo anuwai. Hata hivyo mtafiti alitaka kujua aina mahususi ya kilimo wanachojihusisha nacho watafitiwa nakufahamu kilimo kinachoendelezwa zaidi. Kwa hivyo watafitiwa waliombwa kutaja aina ya kilimo anachojihusisha. Swali la pili katika hojaji ya mtazamaji lilimhitaji kutaja kilimo anachojihusisha nacho. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 5 lifuatalo;

Jed. 5: Kilimo Wanachojihusisha Nacho Watafitiwa

Kilimo	Idadi	Asilimia
Ufugaji wa mifugo	101	38.26
Upanzi wa miche ya chai	142	53.79
Upanzi wa mahindi	31	11.74
Upanzi wa maharagwe	13	4.92
Upanzi wa miwa	4	1.52
Upanzi wa mboga	35	13.26
Upanzi wa matunda	2	0.75
Upanzi wa viazi	12	4.55
Jumla	**264**	**100**

Kwa mujibu wa matokeo katika Jad. 5, asilimia 38.26 (N=101) ya watazamaji wa runinga ya Kass katika kaunti ya Nandi walikubali kushiriki katika ufugaji wa mifugo huku asilimia 53.79 (N=142) wakishiriki katika upanzi wa miche ya chai. Aidha, asilimia 11.74 (N=31) walijihusisha na upanzi wa mahindi tofauti na asilimia 4.92 (N=13) iliyoshiriki katika upanzi wa maharagwe. Wakati huo huo asilimia 1.52 (N=4) ya watazamaji katika kaunti hii walifanya upanzi wa miwa. Kando na upanzi wa miwa, asilimia 13.26% (N=35) ya watazamaji ilishiriki katika upanzi wa mboga. Watazamaji hawa walikiri kupanda mboga kama vile sukuma, kabeji na managu. Isitoshe, asilimia 0.75 (N=2) ilikiri kushiriki katika ukulima wa matunda. Hatimaye, asilimia 4.55 (N=12) ilishiriki katika upanzi wa viazi. Kutokana na matokeo haya ni wazi kwamba watazamaji wa runinga ya Kass katika kaunti ndogo ya Emgwen wanashiriki katika ufugaji wa mifugo na upanzi wa miche ya chai kwa kiwango kikubwa.

Kutokana matokeo haya, inabainika kuwa wanajamii wengi wa kaunti ndogo ya Emgwen wanajihusisha katika ufugaji wa mifugo na upandaji wa miche ya chai. Hii inadhihirisha kuwa wanajamii wa kaunti ndogo ya Emgwen wanategemea kilimo kujiendeza. Hususan upandaji wa miche ya chai na ufugaji wa mifugo. Ugunduzi huu unawiana na maelezo ya Marra (2013) kwamba nchi nyingi ulimwenguni zinategemea kilimo ili kuleta maendeleo. Kwa mujibu wa mtaalamu huyu, nchi ya Chile inatambua kilimo kama sekta muhimu inayoleta maendeleo. Isitoshe, Sekta ya kilimo katika nchi hii huleta ajira kando na kuwasaidia wananchi kujiendeleza.

4.5. Utazamaji wa Vipindi vya Kilimo

Runinga ya Kass huwasilisha vipindi vingi vinavyohusu masuala mbalimbali yanayowaathiri watazamaji. Kati ya masuala haya, suala la kilimo lilibainika kupewa uzito zaidi katika runinga ya Kass kutokana na idadi kubwa ya vipindi ikilinganishwa na vipindi vingine vya masuala mengine ya kijamii. Hali hii ilimpelekea mtafiti kutaka kubaini ni vipindi vipi vya kilimo wanavyopendelea kuvitazama watafitiwa. Baada ya kutumia mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo kuorodhesha vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass, watazamaji walipewa hojaji kutaja kipindi cha kilimo wanachopenda kukitazama. Swali la tatu katika hojaji ya mtazamaji lilitekeleza wajibu huu. Kwa hivyo watafitiwa walipewa fursa ya kutaja kipindi cha kilimo anachopendelea kukitazama. Matokeo yamewasilishwa katika Jed. 6 lifuatalo;

Jed. 6: Utazamaji wa Vipindi vya Kilimo

Kipindi	Idadi	Asilimia
Tugeet ab Kabotik (Sauti ya mkulima)	22	8.33
Mungaret ak Bandaptai (Kilimo biashara na maendeleo)	37	14.02
Longet ab Kabotik (Mkuki wa Mkulima)	49	18.56
Baet ab Kiyakiik (Ufugaji bora wa mifugo)	84	31.82
Boishonik ab Keljin (Kazi zenye faida)	45	17.05
Minet ab bandek (Upandaji wa mahindi)	20	7.56
Temisiet ab chaik (Upandaji wa Miche ya Chai)	77	29.17
Jumla	**264**	**100**

Kutokana na matokeo katika Jed. 6, ilibainika kuwa asilimia 8.33 (N=22) ya watazamaji hutazama kipindi cha Tugeet ab Kabotik (Sauti ya mkulima) huku asilimia 14.02 (N=37) ikikiri kutazama kipindi cha Mungaret ak bandaptai (Kilimo biashara na maendeleo). Aidha, asilimia 18.56 (N=49) ilishadidia kutazama kipindi cha Longet ab kabotik (Mkuki wa mkulima). Kando na asilimia 31.82 (N=84) ya watazamaji waliotazama kipindi cha Baet ab kiyakiik (Ufugaji wa mifugo), asilimia 17.05 (N=45) ya watazamaji walitazama kipindi cha Boishonik ab keljin (Kazi zenye faida). Kipindi cha Minet ab bandek (Upandaji wa mahindi) kilitazamwa na asilimia 7.56 (N=20) huku asilimia 29.17 (N=77) ya watazamaji wakitazama kipindi cha Temisiet ab chaik (Upandaji wa miche ya chai).

Kutokana na matokeo haya ni wazi kwamba wakaazi wa kaunti ndogo ya Emgwen iliyoko kaunti ya Nandi walivitazama vipindi vya ufugaji wa mifugo na upanzi wa miche ya chai kwa asilimia kubwa. Tabia nchi ya kaunti hii huwa nzuri kwa upanzi wa chai na ufugaji wa mifugo. Kipindi cha ufugaji wa mifugo kililenga kuwainua

wanajamii kwa kuwapa mafunzo kuhusu mbinu bora za ufugaji huku upanzi wa miche ya chai kikiwapa mafunzo kuhusu mbinu bora za upanzi wa chai. Matokeo haya yanashadidia ugunduzi wa Okoth (2015) anayedahili kuwa vipindi vinavyowasilishwa kwa lugha za kiasli zinapaswa kulenga kuwainua wanajamii katika nyanja mbalimbali ikiwemo sekta ya kilimo.

4.6. Mchango wa Matumizi ya Kinandi katika Kuihamasisha Jamii kuhusu Ustawi wa Kilimo

Miradi ya kisasa inayokusudiwa kuelimisha umma nchini Kenya haiwezi kueleweka katika lugha nyingine yoyote isipokuwa lugha ya wananchi hao wa vijijini ambao wengi wao hawajui kusoma wala kuandika (Mugambi, 2007). Kutokana na hali hii, mashirika ya serikali na wadau wengine wanastahili kutumia lugha za wenyeji wa vijijini kadri wawezavyo ikiwa wanataka kupata matokeo yenye manufaa. Kwa mujibu wa Mugambi (2007) miradi hii hunuiwa kuwahamasisha wanajamii kuhusu masuala yanayohusu maisha yao. Kutokana na maelezo haya utafiti huu ulitaka kuchunguza jinsi lugha ya Kinandi hutekeleza wajibu huu. Katika kutafiti kuhusu mchango wa lugha ya Kinandi katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo, mtafiti alipata data kutoka kwa watazamaji na watangazaji wa runinga ya Kass. Matokeo ya watazamaji yanawasilishwa katika sehemu ifuatayo baada ya kuzifafanua sifa zao.

4.7. Maoni ya Watangazaji

Vyombo vya habari hutoa fursa kwa watu kujihusisha na kushiriki katika maamuzi na majadiliano kuhusu masuala tofauti yanayoathiri maisha yao (Mohochi, 2006). Kwa mujibu wa Mohochi (2006) vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili huwapa watangazaji fursa nzuri ya kutangamana na wasikilizaji na watazamaji wengi kwa sababu lugha inayotumika ni ile ambayo wanaimudu vyema. Naye, Hymes (1972) katika nadharia ya ethnografia ya mawasiliano anasisitiza kuwa ili kuwe na mafanikio katika mawasiliano, ni sharti lugha inayotumika ilete athari chanya kwa watumiaji. Kwa kuzingatia maelekezo haya, mtafiti alilenga kubaini mchango wa matumizi ya lugha ya Kinandi katika runinga ya Kass kuwasilisha vipindi vya kilimo. Watangazaji na watazamaji walitoa maoni yao kuhusu mchango huu. Watangazaji tisa walihojiwa. Lengo kuu lilikuwa ni kubaini jinsi lugha hii husaidia katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo. Swali la pili katika hojaji ya mtangazaji lilimhitaji mtangazaji kutoa maoni kuhusu mchango wa matumizi ya Kinandi katika kuwasilisha vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 7 lifuatalo:

Jed. 7: Maoni ya Watangazaji

Mchango	Idadi	Asilimia
Ujumbe unaeleweka zaidi	6	66
Watazamaji wanashiriki zaidi	9	100
Watazamaji wanajieleza kwa ujasiri wanapotoa maoni	7	77.78
Kuna upigaji zaidi wa simu kutoka kwa watazamaji	5	55.56
Watazamaji wanapata fursa nzuri ya kupata mafunzo bora kutoka kwa wataalamu waalikwa wa kilimo	4	44.44
Jumla	**9**	**100**

Kutokana na matokeo katika Jed. 7, asilimia 66 (N=6) ya watangazaji walikiri kuwa lugha ya kinandi inapotumika kuwasilisha maudhui ya kilimo, ujumbe hueleweka zaidi na kwa haraka. Kueleweka zaidi na kwa haraka ni madhumuni ya matumizi ya lugha kama inavyoelekeza mhimili wa pili wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972) kwamba matamshi yanayoeleweka na watu wengi katika mazungumzo ndiyo lengo kuu la matumizi ya lugha. Matokeo haya yanashabihiana na matokeo ya Mdee (1999) ambaye alibaini kuwa, mawasiliano yanapotumia lugha ya kitaaluma, mawasiliano hayo hayaeleweki vyema hasa ikiwa yanalenga wakaazi wa mashambani. Anahoji kuwa, watu wengi wanaoshiriki katika kilimo hupatikana katika maeneo ya mashambani ambako lugha za kitaaluma hazifai kutumika katika mawasiliano. Kwa hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa lugha ya Kinandi inapotumika ujumbe unaeleweka zaidi miongoni mwa watazamaji.

Wakati huo huo asilimia 100 (N=9) ya watangazaji walikubali kuwa lugha ya kinandi inapotumika, watazamaji wanashiriki zaidi katika vipindi hivi. Ushiriki huu ulibainika kutokana na upigaji wa simu kutoka kwa watazamaji. Hali hii iliwasaidia watazamaji kupata ufafanuzi wa ziada kuhusu masuala ya kilimo. Matokeo haya yalishabihiana na matokeo ya Orao (2012) katika kipindi cha Tich tire inayowasilishwa kwa lugha ya Dholuo kwamba wasikilizaji wengi walishiriki kwa kupiga simu kwa kuwa walimudu vyema lugha iliyotumika.

Aidha, asilimia 77.78 (N=7) ya watazamaji walisisitiza kuwa lugha hii inapotumika watazamaji wanajieleza zaidi wanapotoa maoni yao katika vipindi hivi. Watazamaji walijieleza zaidi kwa kuwa lugha iliyotumika kuwasilisha masuala ya kilimo ni lugha wanayoimudu vyema na hivyo kufanikisha mawasiliano kama invyelekeza mhimili wa tatu wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972) kwamba lugha inayoeleweka na watu wengi ni nyenzo muhimu katika kufanikisha mawasiliano.

Vile vile, ilibainika kuwa lugha ya Kinandi inapotumika, kuna upigaji zaidi wa simu kutoka kwa wasikilizaji na watazamaji. Hii ilidhihirishwa na asilimia 55.56 (N=6) ya watangazaji. Hatimaye, asilimia 44.44 (N=4) ilithibitisha kuwa lugha ya Kinandi inapotumika, watazamaji wanapata fursa nzuri ya kupata mafunzo kutoka kwa wataalamu waalikwa wa kilimo. Wataalamu hawa hutoa mafunzo ya moja moja kuhusu mbinu bora za kufanikisha kilimo.

4.8. Maoni ya Watazamaji

Vyombo vyote vya habari huwalenga watazamaji katika kuwasilisha vipindi vyao. Hii ina maana kuwa

watazamaji ni kipengele muhimu katika kufanikisha utangazaji kwenye vyombo vya habari (Mokaya, 2020). Aidha, Mwita (2002) akijadili kuhusu umuhimu wa lugha za kiasili anasema kuwa, maendeleo katika jamii hulenga kuyaboresha maisha ya binadamu kwa njia zote lakini lengo hili haliwezi kufikiwa bila matumizi ya lugha. Anahoji kuwa, maendeleo katika sehemu za mashambani yanalenga kuwawezesha watu wengi waishio mashambani kupata huduma muhimu kama vile huduma za afya, elimu na kilimo.

Upataji wa huduma hizi hutegemea mawasiliano bora kupitia vyombo vya habari vinavyotumia lugha za kiasili. Kwa kuzingatia maelezo haya, mtafiti alilenga kubaini mchango wa matumizi ya lugha ya Kinandi kwa watazamaji wa vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass kwa wanajamii wa kaunti ndogo ya Emgwen iliyoko kaunti ya Nandi. Kwa hivyo, watazamaji walilijibu swali la nne kwenye hojaji ya mtazamaji. Swali hili liliwahitaji watazamaji kufafanua mchango wa matumizi ya Kinandi kuwasilisha vipindi vya kilimo kwao kama watazamaji wa vipindi hivi. Matokeo yanawasilishwa katika Jed. 8 lifuatalo;

Jed. 8: Maoni ya Watazamaji

Mchango	Idadi	Asilimia
Ujumbe unaeleweka zaidi	169	64.02
Fursa ya kuuliza maswali kwa undani na kupata majibu ya kina	189	71.59
Fursa ya kujieleza kwa ufasaha	220	83.33
Fursa ya kutangamana na wataalamu wa kilimo	199	75.38
Mbinu za kilimo zinaimarika	260	98.48
Kupatikana kwa soko la bidhaa kwa urahisi	168	63.64
Kunaleta utangamano wa wakulima mbalimbali wanaotumia lugha ya Kinandi	214	81.06
Matumizi ya Kinandi huleta umoja baina ya wakulima	209	79.17
Kunaleta ushirikishwaji wa wakulima wote	223	84.45
Tunapata mafunzo kuhusu kilimo kwa njia rahisi	227	85.99
Wasio na elimu wanapata fursa ya kushiriki	206	78.03
Jumla	**264**	**100**

Kwa mujibu wa matokeo katika Jed. 8, utafiti ulibaini kuwa lugha ya Kinandi inapotumika kuwasilisha vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass, ujumbe unaeleweka kwa urahisi kama inavyoelekezwa na mhimili wa pili wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972). Hii ikiwa asilimia 64.02 (N=169) ya watafitiwa waliohojiwa. Nayo asilimia 71.59 (N=189) ya watafitiwa hawa ilikiri kuwa lugha hii inapotumika wanapata fursa ya kuuliza maswali kwa undani na kupata majibu ya kina.

Asilimia hii inaoana na matokeo ya Misiko (2018) ambaye aligundua kuwa lugha ya Kibukusu inapotumika kuwasilisha masuala ya afya wasikilizaji wa redio ya Sulwe wanapata fursa nzuri ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi zaidi. Wakati huo huo, asilimia 83.33 (N=220) walikubali kuwa, lugha ya Kinandi inapotumika wanapata fursa ya kujieleza kwa ufasaha. Hii ni kwa sababu lugha inayotumika inaeleweka vyema na hivyo kurahisisha mawasiliano kama inavyoelekezwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya ethnografia ya mawasiliano yake Hymes (1972) kwamba madhumuni makuu ya matumizi ya lugha ni kufanikisha mawasiliano. Utangamano bora baina ya wakulima na wataalamu wa kilimo ulibainika kuwa faafu wakati lugha ya Kinandi ilipotumika. Hii ni kwa sababu asilimia 75.38 (N=199) ya wafitiwa walikiri kuwa lugha hii huleta utangamano bora baina yao inapotumika kuwasilisha vipindi vya kilimo. Utangamano huu unapatikana kutokana na mawasiliano bora kama asemavyo Chebet (2020) kwamba wakulima wanaopata mawasiliano bora kuhusiana na masuala ya kilimo huinua viwango vyao vya kilimo. Asilimia 98.48 (N=260) ya watafitiwa walishadidia mchango huu wa lugha ya Kinandi. Soko la bidhaa ni suala muhimu la kuzingatiwa na wakulima wote. Hii ni kwa sababu wakulima wengi hulenga kupata mapato bora kutokana na kilimo chao. Asilimia 63.64 (N=168) ya watafitiwa walikiri kufaidika kupata soko kutokana na matumizi ya lugha ya Kinandi kuwasilisha vipindi vya kilimo huku aslimia 98.48 (N=260) wakikiri kuwa lugha ya Kinandi inapotumika, mbinu zao za kilimo zinaimarika. Matokeo haya yanawiana na ya Abdalla (2022) ambaye aligundua kuwa, maendeleo katika sekta ya kilimo yanawezeshwa na mawasiliano bora baina ya serikali kupitia vyombo vya habari na wakulima. Hali hii ilidhihirika kupitia vipindi vya kilimo vinavyowasilishwa kwa lugha ya Kinandi katika runinga ya Kass.

Aidha asilimia 81.06 (N=214) walikubali kuwa matumizi ya Kinandi huleta utangamano Aidha asilimia 81.06(N=214) walikubali kuwa matumizi ya kinandi huleta utangamanano wakulima mbali mbali wanaotumia lugha ya Kinandi huku asilimia 79.17 (N=209) wakikiri kuwa matumizi ya Kinandi huleta umoja baina ya wakulima. Hali hii ilileta uzalendo na mshikamano katika jamii kama asemavyo Kinoti (2021) kuwa matumizi ya lugha za kiasili huibua hisia za uzalendo miongoni mwa watumiaji. Asilimia 84.45 (N=223) ya watafitiwa walikubali kuwa matumizi ya lugha ya Kinandi huleta ushirikishwaji wa wakulima wote. Kutokana na ushirikishwaji huu, watazamaji wa runinga ya Kass walivifurahia vipindi vya kilimo huku wakiwa na imani na vipindi hivi. Imani hii ya wasikilizaji kwa vituo vya habari huwachochea katika shughuli za maendeleo kama asemavyo (Misiko, 2018). Isitoshe asilimia 85.99 (N=227) walisisitiza kuwa lugha ya Kinandi inapotumika, wao hupata mafunzo kuhusu kilimo kwa njia rahisi. Hii ni kwa sababu lugha inayotumika ni lugha inayoeleweka vyema miongoni mwa watazamaji. Matokeo haya ni sawa na ya Orao (2012) ambaye alibaini kuwa mawasiliano yanayofanywa kwa lugha za kiasili huhakikisha kuwa wakaazi wa mashambani ambao wengi wao ni wakulima hupokea ujumbe kwa njia rahisi.

Hatimaye, asilimia 78.03 (N=206) waliunga mkono msimamo kuwa lugha ya Kinandi inapotumika wasio na elimu wanapata fursa ya kushiriki. Wakulima hawa wanashiriki kwa sababu lugha inayotumika ni lugha yao ya kwanza na wanaimudu vyema. Kwa hivyo mawasiliano kuhusu kilimo yanafanikishwa kwa njia mwafaka kama anavyoelekeza Hymes (1972) katika nadharia ya ethnografia ya mawasiliano.

5. Hitimisho

Utafiti huu ulihusu mchango wa lugha ya Kinandi katika kuihamasisha jamii kuhusu ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya runinga ya Kass katika kaunti ya Nandi. Kabla ya kuchunguza mchango huu, utafiti ulilenga kwanza kubaini lugha wanazozimudu watafitiwa, kilimo wanachojihusisha nacho watafitiwa na vipindi vya kilimo amabavyo hupeperushwa katika runinga ya Kass. Katika kuchunguza mchango wa lugha ya Kinandi, utafiti ulikusanya data kutoka kwa watangazaji na watazamaji.

Ilibainika kuwa asilimia 96.59 (N=255) ya watafitiwa ilimudu lugha ya Kiswahili na Kinandi. Hii ilithibitisha kuwa lugha zinazotumiwa mara nyingi katika mawasiliano baina ya wakaazi wa kaunti ya Nanndi ni Kiswahili na Kinandi. Isitoshe, wakulima wengi katika kaunti hii walijihusisha na upanzi wa miche ya chai. Hii ikiwa asilimia 53.79 (N=142). Kilimo cha chai kilionekana kuwa uti wa mgongo wa wakulima katika kaunti ya Nandi. Kati ya vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass, kipindi cha Baet ab Kiyakiik (Ufugaji wa mifugo) ndicho kipindi kilichotazamwa na idadi kubwa ya watafitiwa. Idadi hii iliwakilishwa na asilimia 31.82 (N=84).

Aidha, asilimia 100 (N=9) ya watangazaji walikubali kuwa kuwa lugha ya Kinandi inapotumika kuwasilisha vipindi vya kilimo, watazamaji wanashiriki zaidi. Hii ni kwa sababu lugha ya Kinandi inaeleweka zaidi miongoni mwao na hivyo basi wanapata fursa kujieleza kwa ufasaha. Wakati huo huo, watazamaji walikiri kuwa lugha ya Kinandi inapotumika kuwasilisha vipindi vya kilimo mbinu zao za kilimo zinaimarika zaidi. Hii ikiwa asilimia 98.48 (N=260). Hii ilitokana na hali kwamba wanakielewa kipindi ipaswavyo. Utafiti huu unapendekeza matumizi zaidi ya lugha asilia katika vyombo vya habari kuimarisha mawasiliano na kuhimiza ukuzaji wa lugha hizo ikiwemo lugha ya Kiswahili.

Marejeleo

Abdalla, N. (2022). Kilimo na Kilimo Mseto. Hali Halisi na Mapendekezo ya Maboresho katika Sera za Taifa. Dar es Salaam. East African Scholars Publishers.

Ary, D. na wenzake. (1972). Introduction to Research in Education. New York: Holtrine and Winston Publishers.

Chebet, N. (2020). Dhima ya Umahuluti wa Utamaduni katika Uamilishaji wa nyimbo za harusi miongoni mwa Wanandi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Moi (Unpublished).

Hymes, D. (1972). Models for the Interaction of Language and Social Life. In J.J. Gumperz & D.H. Hymes (Eds.), Directions in sociolinguistics: The Ethnography of Communication (pp. 35-71). New York: Holt, Rinehart and Winston.

KHRC. (2008). Ballots to Bullets. Organised Political Violence and Kenyans Crisis of Governance. Nairobi. Government printers.

Kandagor, M., & Toboso, M., (2021). Utandawazi Kama Tishio kwa Lugha za Kiafrika. Katika Mauka, L, Jebet A,. & Kyeu D., (Wah). Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika. Chuo Kikuu cha Moi (Kur 70-75).

Kinoti, W. (2021). Mchango wa Lugha za Kiasili katika Ufikiwaji wa Maendeleo Endelevu. Embu: East Africa Scholars Publishers.

Marra, S. (2013). Language Skills and Innovation in Global Agriculture. Madrid. Madrid Publishers

Misiko, W. (2018). Lugha kama Rasilmali ya Jamii: Uchunhuzi wa Redio za FM zibazotumia Kibukusu katika Kaunti ya Bungoma. Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).Mutenyo, A. (2022). Kiswahili na Maendeleo ya Kilimo: Chuo Kikuu cha Kabale. Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa).

Mdee, J. S. (1999). Matumizi ya Istilahi katika Kiswahili na Jinsi Yanavyoathiri

Mohochi, E. S. (2006). Kiswahili na Vyombo Vya Habari Nchini Kenya: Makosa

Mokaya,M.(2020).Language Policy and Practices in Education in Kenya and Uganda: Perception of Parents, Pupils and Teachers on the use of Mothertongue. Nairobi: Phoenix Publishers.

Mwita,B. M. (2002). Rural Development in Kenya: Is Kiswahili The Language of

Mutenyo, A. (2022). Kiswahili na Maendeleo ya Kilimo: Chuo Kikuu cha Kabale. Tasnifu ya Uzamili. (Haijachapishwa)

Mugambi,P.(2007). Kutumia utofauti wa Lugha ili kuleta Maendeleo ya Kitaifa na Maeneo. Katika Senkoro,F.E.M.K(mh).Lugha na Fasihi ya Kiswahili,Afrika Mashariki, Kur. 45-53.Dar es Salaam.CHAKAMA.

Muthwii, M. (2002). Language Policy and Practices in Education in Kenya and Uganda: Perception of Parents, Pupils and Teacher on the Use of Mother Tongue. Nairobi: Phoenix Publishers.

Okoth, A. (2015). The Emergence and Growth of Vernacular Radio in Kenya: A Case study of Ramogi Radio. Kenyatta University. M.A Thesis (Unpublished).

Orao, J. (2012). The Kenyan Indeginous Languages and the Mass Media: Challenges and Opportunities. Nairobi: Longhorn Publishers.

Raitania, M.A (2014). Mikakati ya upole katika vipindi vya runinga: mawaidha ya Bi.Msafwari katika runinga ya citizen.Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.

Samoei, N. (2015). The Influence of Kass fm in the

Promotion of Food Security among Tugen in Perkerra. Master Thesis. University of Nairobi (Unpublished).